

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA SABA

16 APRILI, 2024



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA SABA – TAREHE 16 APRILI, 2024

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

79. MHESHIMIWA JAFARI WAMBURA CHEGE (RORYA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka Jokofu katika Kituo cha Afya cha Kinesi - Rorya ili Mochwari ianze kutoa huduma.

80. MHESHIMIWA DANIEL AWACK TLEMAI (KARATU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatoa fedha za ukarabati wa Kituo cha Afya Oldeani.

81. MHESHIMIWA ANATROPIA LWEHIKILA THEONEST (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, fedha kiasi gani imepatikana kama kodi ya mauzo ya Kahawa, Ndizi, Maharage na Mahindi katika Mkoa wa Kagera kwa Mwaka 2010 - 2023.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

82. MHESHIMIWA ESTHER EDWIN MALLEKO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, kuna mpango gani wa kuwasaidia Wajasiriamali kuzalisha bidhaa bora na kupata masoko ya uhakika.

WIZARA YA UJENZI:

83. MHESHIMIWA JACQUELINE NGONYANI MSONGOZI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Daraja la Mitomoni linalounganisha Wilaya ya Songea na Nyasa.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

84. MHESHIMIWA AMINA DAUD HASSAN (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Watalii wangapi wameingia nchini tangu kufanyika kwa *Royal Tour* iliyoasisiwa na Mheshimiwa Rais ili kuitangaza nchi yetu.

**85. MHESHIMIWA KILUMBE SHABANI NG'ENDA
(KIGOMA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka Vivutio vya Utalii katika Mji wa Ujiji ili Watu mbalimbali Duniani watembelee.

WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

**86. MHESHIMIWA MICHAEL MWITA KEMBAKI
(TARIME MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga Uwanja wa Michezo Wilaya ya Tarime.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

**87. MHESHIMIWA JESCA JONATHANI
MSAMBATAVANGU (IRINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kuwasaidia Machinga wa Iringa Mjini Shilingi Milioni 700 kwa ajili ya kuboresha mazingira yao.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

88. MHESHIMIWA STANSLAUS SHING'OMA MABULA (NYAMAGANA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuimarisha utoaji wa huduma kwenye Zahanati zinazomilikiwa na Jeshi la Polisi.

89. MHESHIMIWA ASHA ABDULLAH JUMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali inadhibiti vipi suala la vyombo vya usafiri wa umbali mrefu kusimamishwa barabarani mara kwa mara.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

90. MHESHIMIWA JOSEPHAT SINKAMBA KANDEGE (KALAMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, nini mpango wa Serikali wa kujenga na kukarabati Mahakama za Mwanzo Wilayani Kalambo.

WIZARA YA UCHUKUZI:

91. MHESHIMIWA MOHAMED SAID ISSA (KONDE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaondoa Mbwa wanaokagua mizigo katika Meli za Abiria Bandari ya Dar es Salaam kwenda Zanzibar kwa kuwa siyo rafiki kwa abiria.

92. MHESHIMIWA SUBIRA KHAMIS MGALU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, mpango wa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo na eneo la viwanda Bagamoyo umefikia hatua gani ya utelekezaji.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

DODOMA
16 APRILI, 2024

N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE

